IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

N04/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 2 November 2004 (morning)
Mardi 2 novembre 2004 (matin)
Martes 2 de noviembre de 2004 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas ce livret avant d’y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# BINADAMU NA PAKA

❶ Huku Kamau akila kipande cha sima na sukumawiki za kuchemshwa, fikira zilikuwa zampukutisha machozi. Alisikitishwa na hali ya maisha yake. Aliyaona hayakuwa na matumaini yoyote. Kesho yake aliiona imehanikiza giza totoro. Yu wapi babake? Yu wapi mamake? Alitamani kusema nao lakini ole wake! Wazazi wake walikuwa wamefunga safari isiyo na marejeo. Kamwe hatawaona tena! Walimwachia jukumu la kuendesha maisha yake na ya nduguze bila uongozi. Alikuwa mwana na wakati huohuo, alikuwa mzazi. Na urithi wake? Hakuwa na urithi wowote isipokuwa shida.

❷ Juma lililopita, Kamau alipata nafasi ya Kwenda kumtembelea Tovu kwake na kumwomba msaada. Tovu alikuwa mwajiri wa marehemu babake Kamau, na Kamau aliamini angepata msaada kutoka kwake. Akamwendea. Alipokuwa sebuleni kwa Tovu alipata nafasi ya kuona starehe iliyomzingira. Jicho lake lilikuwa likiduruduru kila pembe, akawa anashangazwa na kiasi cha uzuri wa kila kilichokuwemo. Ama kweli kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Bahati haikusimama. Licha ya utajiri mwingi aliokuwa nao, Tovu alikataa katakata kumwonea huruma Kamau. Kwa upande wake, Kamau alipigwa na butwaa kwa kuona kile alichokuwa hajakiona mbeleni. Kumbe, licha ya idhilali iliyomwelemea kila uchao, mlikuwa na wengine walioishi raha mustarehe wakila na wakinywa watakacho na wakisaza watakavyo? Alijiona kama binadamu asiyekamilika.

❸ Nyau! Nyau! Mkondo wa fikira zake ulikatizwa ghafla na paka wake aliyekondeana. Alimrushia paka yule kipande cha sima asiendelee kulia kwa sauti ya masikitiko. Kwa hakika, Kamau hakuona tofauti yoyote baina yake na paka yule. Alimwonea imani kwa vile alivyodhilika japo kuna wakati akimhusudu kwa kuzaliwa paka wala sio binadamu. Fikra kama hizi zilimjia Kamau mara kwa mara, akasahau kwamba binadamu ana sifa nyingi, sifa ambazo lau angalikuwa paka, hangalikuwa nazo. Chukulia sifa kama ya uundaji. Sifa hii inampambanua binadamu na wanyama wengine. Binadamu ndiye kiumbe wa pekee anayeweza kutumia ubunifu akaunda vitu mbalimbali kama mashine, vyombo vya baharini, umeme, viwanda na majengo ya kila aina. Isitoshe, binadamu anaweza, kwa kiasi kikubwa, kuyaunda maisha yake kama atakavyo. Anaweza kuunda ndege itakayomsaidia kuchunguza sayari za kila aina; anaweza kuunda meli inayohimili dhoruba kubwa; anaweza pia kuunda tarakilishi (kompyuta) itakayomrahisishia kazi yake. Binadamu ana uwezo wa kufikiri, kupanga, kuzungumza na wenzake, kupika chakula chake, kujifunza lugha za binadamu wenzake, kutenda mambo mengi kwa kukusudia, na mengine mengi. Anaweza hata kujifanya mnyama kitabia akiamua kufanya hivyo. Almuradi, binadamu amepewa uwezo wa kufinyanga maisha yake kulingana na mazingira yake. Paka hana kipawa hiki.

❹ Kamau alisahau kwamba binadamu ni kiumbe awezaye, kwa kutumia nguvu zake na akili yake, kubadilisha mazingira na maisha yake. Baada ya kuketi na kuisikitikia hali yake, ilimbidi Kamau aamke na aanze kutafuta njia mpya za kuyabadilisha maisha yake na ya nduguze.

**KIFUNGU B**

# UMEME NGUZO MUHIMU YA MAENDELEO KWA WATANZANIA

Hivi sasa dunia imekuwa katika mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia.

Mabadiliko hayo yamekuwa yakigusa sekta mbalimbali, ikiwemo sekta ya nishati.

Hapa Tanzania kwa kipindi cha muda mrefu Watanzania walizoea kutumia umeme unaosambazwa na shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Hata hivyo, huduma ya umeme inayotolewa na TANESCO, haitoshelezi watumiaji wote hasa wale wa maeneo ya vijijini.

Inaelezwa kuwa asilimia 90 ya nyumba hapa nchini hazijaunganishiwa umeme lakini kwa kuzingatia umuhimu wa huduma hiyo na watu wake, kampuni mbalimbali zimeamua kufanya mapinduzi kwa ajili ya kuwasaidia watu wengi zaidi wanaohitaji huduma ya umeme.

Mabadiliko yanaweza kuonekana hivi sasa hasa baada ya makampuni mbalimbali kuamua kuzalisha na kusambaza mfumo wa umeme utokanao na mionzi ya jua na gesi asilia.

Aina hii ya mifumo ya Kuzalisha umeme inapatikana kwa urahisi na huweza kutumika katika maeneo mbalimbali, hasa kwa watu wa vijijini ambao hawana uwezo wa kuunganisha umeme wa TANESCO.

Gharama ya kuunganishia umeme wa mionzi ya jua na ya utunzaji ni ndogo ukilinganisha na umeme wa kawaida. Mbali na hivyo mtumiaji ana uwezo wa kutumia umeme huo kwa zaidi ya miaka 20.

Mbali na haya umeme utokanao na gesi asilia ni safi, wa uhakika, salama na rahisi kutumia, pamoja na hivyo hakuna madhara kwa mazingira na watu wanaoishi karibu na maeneo litakapopita bomba linalopitishia gesi hiyo.

Katika toleo hili kampuni mbalimbali zinaeleza malengo, mafanikio na namna zinavyotoa huduma, ili kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na uwezo wa kutumia umeme wakati wowote na kwa bei nafuu.

**KIFUNGU C**

# WEMA

❶ Mtu akiwa mwema mbele ya Maulana hukumbuka daima kwamba wema wote watoka kwake, na kwamba Mola ndiye hakimu wa watu wote, mwenye kuwapenda matajiri na maskini. Vile Rabana anavyomsaidia kila adinasi, na sisi pia ni lazima tuwasaidie mahuluki wote kadiri tuwezavyo. Kufanya vile huitwa ukarimu.

❷ Kumwona mja maskini hana nguo, utampa vazi lolote lililo la ziada kwako, apate la kujisetiri. Lakini halafu haifai kutangaza na kunadi kadmnasi ya watu kwamba mtu fulani nimempa hiki na kile.

❸ Endapo mtu hana mahali pa kulala, nawe maskani yako yana nafasi, utamwita ukamwonyeshe chumba cha kulala bila kumtoza kodi, na hata maakuli utampa bila malipo. Ukarimu huo ni mzuri sana, lakini mkarimiwa usiwe mtu wa kutendewa uwezapo kuepa, ila uwe mtu wa kutendea. Afadhali kutendea kuliko kutendewa.

❹ Na mgeni akishapokelewa katika nyumba, na amekaa siku mbili tatu, desturi kumsaidia mwenyeji katika kazi, kulima ama kujenga ama kazi yoyote iliyoko. Lakini awapo yu mvivu na mzembe, hataki kazi ila kula na kulala, watu humtolea maneno ya fumbo, husema: Mno ni mno! U mzigo! Maana yake ufunganye virago uende kwani akufukuzaye hakwambii toka. Nao wema usizidi uwezo.

**KIFUNGU D**

# KENYA YAJITUTUMUA KATIKA MICHEZO YA NDONDI, RIADHA.

## Yatwaa Medali Nne Za Dhahabu, Abuja, Nigeria.

Kenya juzi ilifanikiwa kupata medali nne za dhahabu katika michezo ya Afrika kupitia katika michuano ya ndondi na riadha.

Bondia Sulemain Bilali alikuwa wa kwanza kuipatia Kenya medali ya dhahabu baada ya kumdunda kwa pointi Ecepheth Endekaichen wa Ethiopia katika pambano la uzani wa fly.

Akizungumza baada ya pambano hilo, Bilali alisema ilikuwa fahari kwake kumdunda Ecephath kwa vile ni bondia mzuri.

Aliongeza kuwa ushindi wake pia ulileta faraja kwa Kenya kwa vile ilikuwa medali ya kwanza ya dhahabu baada ya wanariadha wa nchi hiyo kuvurunda katika mbio za mita 10,000 na 5,000.

Saa chache baadaye, mwanariadha Ezra Sambu aliiongezea Kenya medali ya pili ya dhahabu baada ya kushinda mbio za mita 400 kwa wanaume kabla ya Ezekiel Kemboi kushinda mbio za mita 3,000 kuruka viunzi.

Mary Nakhumicha aliiongezea Kenya medali ya nne baada ya kushinda mchezo wa kurusha mkuki.

Paul Koech aliiwezesha Kenya kupata medali ya fedha katika mbio za mita 3,000 kuruka viunzi baada ya kuibuka mshindi wa pili. Medali ya Shaba ilinyakuliwa na Tewodoros Shiferaw wa Ethiopia.

Katika mbio za mita 1,500 kwa wanawake, Jacquiline Maranga wa Kenya alitwaa medali ya fedha baada ya kuibuka mshindi wa pili akifuatiwa na nduguye Naomi Mugo. Mshindi wa mbio hizo alikuwa Kutre Durecha wa Ethiopia.

Justus Koech wa Kenya alishindwa kutamba katika mbio za mita 800 kwa wanaume baada ya kuibuka mshindi wa tatu na kutwaa medali ya shaba.

Wanariadha wa Ethiopia walitamba katika mbio za mita 5,000 na 10,000 baada ya kuibuka washindi na kutwaa medali za dhahabu.

Sileshe Sihene aliibuka mshindi wa mbio za mita 5,000 kwa kutumia dakika 27: 42.13 wakati Gebreagziabher Gebremariam alishinda mbio za mita 10,000.